# THE IMPLEMENTATION OF THE NATIONAL PROGRAMME FOR FOOD SELF-SUFFICIENCY ACT, 1988.

## ARRANGEMENT OF SECTIONS

SECTION


1. Short title and Commencement.
2. Application.
3. Interpretation.
4. Establishment and Implementation of the Programme.
5. Committee for the overall supervision of the Programme.
6. Committee of Experts.
7. Programme Implementation Committees.
8. Composition of Regional Programme Implementation Committee.
9. Composition of District Programme Implementation Committee.
10. Composition of the Constituent Programme Implementation Committee.
11. Functions of the Committees.
12. Establishment functions and composition of Secretariat.
13. Technical advices.
14. Meeting procedure and quorum.
15. Registration.
16. Identification.
17. Offences.
18. Regulations.
19. Repeal of Decree No.2 of 1974.

ACT NO.3 OF 1988

I ASSENT,

Idris Abdul Wakil

IDRIS ABDUL WAKIL
PRESIDENT OF ZANZIBAR
AND
CHAIRMAN OF THE REVOLUTIONARY
COUNCIL.

..........15 August,....... 1988.

AN ACT TO REPEAL AN INCREASE IN AGRICULTURAL PRODUCTION DECREE, 1974 AND TO ENACT A LAW FOR THE ESTABLISHMENT OF THE NATIONAL PROGRAMME FOR FOOD SELF-SUFFICIENCY IN ZANZIBAR, PROVIDE FOR ITS IMPLEMENTATION AND TO ENSURE THAT EVERY ABLE-BODIED PERSON ENGAGED IN THE IMPLEMENTATION OF THE FOOD SELF-SUFFICIENCY PROGRAMME IN PRACTICE AND PRODUCTIVITY AND TO PROVIDE FOR OTHER MATTERS CONNECTED THEREWITH AND INCIDENTAL THERETO.

ENACTED BY THE HOUSE OF REPRESENTATIVES OF ZANZIBAR.

Short title and commencement.

1. This Act may be cited as the Implementation of the National Programme for Food Self-Sufficiency Act, 1988 entitled in Kiswahili "Sheria ya Mpango wa Taifa wa Kujitosheleza kwa Chakula, (MTAKULA) ya Mwaka 1988", and shall come into operation on such date as the Minister may by notice in the Gazette appoint.

Application.

2. This Act applies to all persons resident in Zanzibar and shall not apply to any person who is -

(a) under fifteen years of age;

(b) certified by a doctor to be incapable of working due to old age, illness or infirmity;

2/....

(c) a full time student in an institution of learning;

(d) exempted by the Minister in an Order published in the Gazette.

Interpretation.

3. In this Act, unless the context otherwise requires -

"Committee" means the Committee established under sections 5 and 7 of this Act;

"Zone" means the region, District or Constituency as the case may be established by the Local Government Act, No.3 of 1986;

"Director" means the Director responsible for agriculture and includes any person appointed in that capacity;

"Government" means the Revolutionary Government of Zanzibar;

"Minister" means the Minister for the time being responsible for agriculture in Zanzibar;

"Programme" means the National Programme for Food Self-Sufficiency in Zanzibar abbreviated in Kiswahili MTAKULA, established under section 4 of this Act;

"Party" means Chama cha Mapinduzi.

Establishment and Implementation of the Programme.

4.(1) There is hereby established a programme to be known as the National Programme for the Food Self-Sufficiency.

(2) The programme shall be implemented at the level of Central as well as Local Government.

Committee for the overall supervision of the programmed.

5.(1) For the purpose of facilitating control and ensuring the implementation of the programme aimed at maintaining self-sufficiency in food, there is hereby established a National Committee for the overall supervision of the Programme which shall consist of :-

(a) The Chief Minister as Chairman;

(b) Ministers responsible for -

(i) Regional Administration;

(ii) Finance and Planning;

(iii) Agriculture, Livestock and Natural Resources;

(iv) Trade and Industries;

(v) Water, Construction and Energy,

as members;

(c) all Regional Commissioners as members;

(d) all Regional Party Secretaries as members;

(e) Deputy Secretary General of Washirika as a member;

(f) the Mayor of Zanzibar as a member; and

(g) the Principal Secretary to the Ministry of Agriculture, Livestock and Natural Resources shall be the Secretary to the Committee.

(2) The National Committee shall be responsible for the overall supervision of the programme and in particular it will:

(a) ensure that sufficient agricultural land is made available for cultivation and that allocation of land is made in accordance with overall production plan;

(b) lay out plans of the programme and devise strategy for its implementation and ensure the availability of all vital services as may be necessary for the successful implementation of the programme;

(c) fix agricultural target for any particular year;

(d) direct the type of cash crops to be grown in areas not utilized for food crops;

(e) to ensure the availability of all purpose services at regional, district and constituency levels with specific reference to the use of fertilizers, insecticides, pesticides and other modern methods of cultivation which will result in increased production;

(f) generally advise the Government on the best ways of attaining the objects of this Act.

Committee of experts.

6.(1) There shall be a Committee of experts which shall consist of :

(a) Principal Secretary to the Chief Minister's Office as member;

(b) Principal Secretary to the Ministry of Agriculture, Livestock and Natural Resources as Secretary;

(c) Principal Secretary to the Ministry of Finance and Planning as member;

(d) Principal Secretary to the Ministry of Trade and Industry as member;

(e) Principal Secretary to the Ministry of Water, Construction and Energy as member;

(f) all Regional Administrative Officers as members.

(2) The functions of the Committee of Experts shall be :-

(a) to advise the National Committee and give expert opinion on matters related with and incidental to the implementation of the programme;

(b) to prepare agenda for the meetings of the National Committee;

(c) to co-ordinate progress of different Committees on the programme.

5/....

Programme Implementation Committees.

7.(1) There shall be a Programme Implementation Committee at the region, district and constituency levels.

(2) The Minister may by notice in the Gazette establish any other Committee for the better carrying out of the objectives of this Act.

Composition of Regional Programme Implementation Committee.

8. The Regional Programme Implementation Committee in every region shall consist of:

(a) Regional Commissioner as Chairman;

(b) Regional Party Secretary as member;

(c) All District Commissioners in that region as members;

(d) Secretary to the Party Regional Executive Committee on Economic and Planning Affairs as member;

(e) Members of the House of Representatives from that Region as members;

(f) Members of Parliament from the regions as members;

(g) Councillors of the Constituent Governments from each Constituency in the region as members;

(h) Regional Secretary of Washirika as member;

(i) Regional Agricultural Livestock and Natural Resources Officer as Secretary.

Composition of District Programme Implementation Committee.

9. The District Programme Implementation Committee in each District shall consist of :-

(a) District Commissioner as Chairman;

(b) Party District Secretary as member;

(c) Chairman of the Town Council as member;

(d) Two members of the House of Representatives in the District as members;

(e) two members of Parliament in the District as members;

(f) Secretary to the Party District Executive Committee on Economic and Planning Affairs as member;

(g) District Secretary of Washirika as member; and

(h) District Agricultural, Livestock and Natural Resources Officer of that District as Secretary.

Composition of the Constituent Programme Implementation Committee.

10. The Constituent Programme Implementation Committee in each constituency shall consist of:

(a) Councillor of a Constituent Government as Chairman;

(b) A member of Parliament in that constituency as member;

(c) A member of the House of Representatives in that constituency as member;

(d) CCM Branch Secretaries in that constituency as members;

(e). Representatives of a Constituent Government from each Branch as members;

(f) Agricultural and Livestock Officer in that constituency as Secretary.

Functions of the Committees.

11. Every Programme Implementation Committee shall be responsible for the efficient implementation of the provisions of this Act within their respective zones and in particular shall:

(a) ensure that all available land within their zone or jurisdiction is cultivated in accordance with the plan with a view to achieving the set targets;

(b) ensure that the production targets within their zone of supervision is being met;

7/....

(c) supply the Committee above it progress reports on the agricultural activity undertaken, achievements or shortcomings taking place within their zone;

(d) co-operate with all other Committees, Party or Government organs in the task of ensuring production, harvesting, collection and marketing of agricultural produce; and

(e) take adequate precautions to protect crops from theft, damage or destruction.

Establishment functions and composition of Secretariat.

12.(1) There is hereby established a Secretariat to be known as Co-ordinating Secretariat. Its functions shall be to co-ordinate and liaise with other Committees in relation to the programme and procedures towards implementation of that Programme.

(2) The Secretariat shall consist of :-

(a) Principal Secretary, Ministry of Agriculture, Livestock and Natural Resources as Chairman;

(b) Head of the Extension Services as Secretary;

(c) Directors of Agriculture, Livestock Forestry, Fisheries and National Resources as members;

(d) Officer in Charge, Ministry of Agriculture, Livestock and Natural Resources, Pemba as member.

Technical advices.

13. Subject to any other written law the Agricultural and Livestock Officer, fisheries officer and forestry officer may give technical advice in the implementation of the programme to any person engaged in the programme.

8/....

Meeting procedure and quorum.

14. The Committee and the Secretariat shall regulate its own procedures:

Provided that the quorum at any meeting of the Committee or Secretariat shall be more than half the members.

Registration.

15.(1) Without prejudice to any written law and for the purpose of facilitating the implementation of this programme the Minister shall cause to be established and maintained a register of all able-bodied persons not exempted from the implementation of this programme under section 2 of this Act and who are resident in Zanzibar.

(2) There shall be entered in respect of every such resident the following particulars :-

(i) the name of resident;

(ii) address;

(iii) age;

(iv) number of dependants if any;

(v) present employment/engagement if any;

(vi) present residence;

(vii) nationality;

(viii) original or adopted domicile.

(3) The Register shall be kept in such a form and entries in it and removal from it shall be made in such a manner as the Minister may prescribe.

(4) The District Commissioner, District Administrative Officer, or any other specified officer appointed by the Minister shall supervise the Registration of Residents in their Districts.

Identification.

16. Subject to any other written law, the Minister may make regulations prescribing the manner in which the person who is duly registered and engaged in the implementation of the programme may be issued with identification card.

Offences.

17. Any person who fails to comply with the provisions of this Act or who encourages another person to contravene the provisions of this Act or who by any wilful act frustrates the aims and objects of this Act shall be guilty of an offence and if convicted by the court shall:

be sent to an educational centre for a period not exceeding two years or to a fine not exceeding five thousand shillings or to both such fine and committal to an educational centre.

Regulations.

18.(1) The Minister may make regulations for the better carrying out of the provisions of this Act.

(2) The Minister may delegate his authority to local Government to make by-laws for the purpose of attaining the objects of this Act within their zones.

Repeal of Decree No.2 of 1974.

19. The Increase in Agricultural Production Decree, No.2 of 1974 is hereby repealed.

Passed in the House of Representatives of Zanzibar on the 18th day of June, 1988.

Abdul Rahman Ali Saleh
ABDUL RAHMAN ALI SALEH
CLERK TO THE HOUSE OF
REPRESENTATIVES OF ZANZIBAR.

SHERIA NAMBA 3 YA 1988

NAKUBALI

Sd. I. A WAKIL.

IDRIS ABDUL WAKIL
RAIS WA ZANZIBAR
NA
MWENYEKITI WA BARAZA LA MAPINDUZI

.......15.....OGASTI..., 1989

SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA UONGEZAJI WA MAZAO YA KILIMO YA MWAKA 1974 NA KUWEKA SHERIA YA KUANZISHA MPANGO WA TAIFA WA KUJITOSHELEZA KWA CHAKULA ZANZIBAR, KUNADHIMU UTEKELEZAJI NA KUHAKIKISHA KILA MTU MWENYE UWEZO WA KUFANYAKAZI ANASHIRIKI KIKAMILIFU KATIKA MPANGO HUO, PAMOJA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO.

---

IMETUNGWA NA BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR.

Jina fupi na tarehe ya kuanza

1. Sheria hii itajulikana kama Sheria ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa kujitosheleza kwa chakula (MTAKULA) ya mwaka 1988 na itaanza kutumika rasmi tarehe itakayotolewa na Waziri kwenye Gazeti rasmi la Serikali.

Matumizi

2. Sheria hii itatumika kwa watu wote ambao ni wakaazi wa Zanzibar na haitotumika kwa mtu yeyote ambae:-

2/.....

(a) ana umri chini ya miaka kumi na tano;

(b) amethibitishwa na daktari kuwa hawezi kufanya kazi kwa sababu ya uzee, ugonjwa au udhaifu wa aina yoyote;

(c) ni mwanafunzi wa kudumu katika Taasisi zinazotoa taaluma;

(d) amesamehewa na Waziri kwa kutoa Tangazo Gazetini;

Ufafanuzi

3. Katika Sheria hii isipokuwa vyenginevyo itakavyoelezwa:-

"Kamati" ina maana Kamati iliyoanzishwa chini ya Kifungu cha 5 na 7 cha Sheria hii;

"Kanda" ina maana Wilaya, Mkoa au Jimbo lililoanzishwa na Sheria ya Serikali ya Mitaa Namba 3 ya 1986 (Local Government Act, No.3) kama hali itakavyokuwa;

"Mkurugenzi" ina maana Mkurugenzi anaehusika na mambo ya Kilimo na inajumuisha mtu yeyote aliechaguliwa kushika uwezo huo;

"Waziri" ina maana Waziri anaehusika na Kilimo/Mifugo kwa Zanzibar;

"Serikali" ina maana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Mpango" ina maana Mpango wa Taifa wa kujitosheleza kwa Chakula Zanzibar "MTAKULA" ulioanzishwa chini ya Kifungu cha 4 cha Sheria hii;

3/.....

"Chama" ina maana Chama cha Mapinduzi;

Uanzishwaji na Ufanikishaji wa mpango

4.(1) Unaansishwa Mpango utaojulikana kama Mpango wa Taifa wa kujitosheleza kwa Chakula "MTAKULA";

(2) Mpango huu utatekelezwa katika ngazi zote za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Kamati ya Kusimamia utekelezaji wa Mpango

5.(1) Kwa madhumuni ya kurahisisha utekelezaji wa mpango wa kujitosheleza kwa Chakula, inaanzishwa Kamati ya Taifa ya kusimamia utekelezaji wa mpango huo itayokuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Waziri Kiongozi kama Mwenyekiti;

(b) Mawaziri watakaokuwa na dhamana zifuatazo:-

(i) Tawala za Mikoa;

(ii) Fedha na Mipango;

(iii) Kilimo, Mifugo na Maliasili;

(iv) Biashara na Viwanda;

(v) Maji, Ujenzi na Nishati kama wajumbe;

(c) Wakuu wa Mikoa wote kama wajumbe;

(d) Makatibu wote wa Chama wa Mikoa kama wajumbe;

(e) Msaidizi Katibu Mkuu wa Washirika kama Mjumbe;

(f) Meya wa Mji wa Zanzibar kama Mjumbe; na

(g) Katibu Mkuu - Kilimo, Mifugo na Maliasili ambae atakuwa Katibu wa Kamati;

(2) Kazi za Kamati ya Taifa itakuwa ni usimamizi wa Mpango wa MTAKULA na zaidi:-

(a) Kuhakikisha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya Kilimo na kwamba ugawaji wa ardhi utafanyika kulingana na malengo ya uzalishaji;

(b) Kuandaa taratibu za mpango wa MTAKULA na kutafuta mbinu za utekelezaji wake na kuhakikisha upatikanaji wa mahitaji yote muhimu kwa ufanikishaji wa mpango huo.

(c) Kuweka malengo ya uzalishaji wa mazao kwa mwaka;

(d) Kuongoza ni mazao gani ya biashara yapandwe katika maeneo ambayo hayatumiki kwa mazao ya chakula;

(e) Kuhakikisha upatikanaji wa huduma zote muhimu za kilimo katika ngazi zote kuanzia Mikoa, Wilaya mpaka katika Majimbo na zaidi kutilia mkazo matumizi ya madawa ya kuulia wadudu na wanyama waharibifu kwa vipando au mazao kwa lengo la kuhakikisha uengezekaji wa mazao;

(f) Kuishauri Serikali kwa jumla juu ya njia bora ya kufanikisha malengo yaliyomo katika Sheria hii;

Kamati ya Wataalamu

6.(1) Kutakuwa na Kamati ya Wataalamu wa MTAKULA itakayokuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Katibu Mkuu - Afisi ya Waziri Kiongozi kama Mwenyekiti;

(b) Katibu Mkuu - Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili kama Katibu;

(c) Katibu Mkuu - Wizara ya Fedha na Mipango kama Mjumbe;

(d) Katibu Mkuu - Wizara ya Biashara na Viwanda kama Mjumbe;

(e) Katibu Mkuu - Wizara ya Maji, Ujenzi na Nishati kama Mjumbe;

(f) Afisa Tawala wa kila Mkoa kama Wajumbe;

(2) Kazi ya Kamati ya Wataalamu wa MTAKULA itakuwa:-

(a) Kuisaidia Kamati ya Taifa kwa kutoa ushauri wa kitaalamu;

(b) Kutayarisha agenda za Mikutano ya Kamati ya Taifa;

(c) Kuratibu Maendeleo ya Kamati mbali mbali zinazohusika na MTAKULA.

Kamati za Utekelezaji

7.(1) Kutakuwa na Kamati za utekelezaji wa kilimo katika kila Mkoa, Wilaya na Jimbo.

(2) Waziri kwa kutangaza katika Gazeti Rasmi la Serikali atakuwa na uwezo wa kuanzisha Kamati nyengine yoyote zaidi ya Kamati ya utekelezaji kwa madhumuni ya utekelezaji wa malengo yaliyomo katika Sheria hii.

Muundo wa Kamati ya Utekelezaji ya Mkoa

8. Kamati ya utekelezaji wa kilimo ya Mkoa itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mkuu wa Mkoa kama Mwenyekiti;

(b) Katibu wa Chama wa Mkoa kama Mjumbe;

(c) Wakuu wa Wilaya wote wa Mkoa huo kama wajumbe;

(d) Katibu wa Idara ya Uchumi wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Taifa, kama Mjumbe;

(e) Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa Mkoa huo kama Wajumbe;

(f) Wajumbe wa Bunge wa Mikoa kama Wajumbe;

(g) Madiwani wa Serikali za Mitaa wa kila Jimbo wa Mkoa huo kama Wajumbe;

(h) Katibu wa Mkoa wa Washirika kama Wajumbe;

(i) Afisa wa Kilimo na Mifugo wa Mkoa huo kama Katibu;

Muundo wa Kamati ya Utekelezaji wa Kilimo ya Wilaya

9. Kamati ya utekelezaji wa kilimo ya kila Wilaya itakuwa na Wajumbe wafuatao:-

(a) Mkuu wa Wilaya kama Mwenyekiti;

(b) Katibu wa Chama (CCM) wa Wilaya kama Mjumbe;

(c) Mwenyekiti wa Baraza la Mji kama Mjumbe;

7/.....

(d) Wajumbe wawili wa Baraza la Wawakilishi wa Wilaya kama Wajumbe;

(e) Wabunge wawili waliomo katika Wilaya hiyo;

(f) Katibu wa Idara ya Uchumi wa Sekretarieti ya Halmashauri Kuu ya Wilaya kama Mjumbe;

(g) Katibu wa Wilaya wa Washirika kama Mjumbe; na

(h) Afisa wa Kilimo, Mifugo na Maliasili wa Wilaya hiyo kama Katibu.

Muundo wa Kamati ya Jimbo

10. Kamati ya Jimbo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Diwani wa Jimbo kama Mwenyekiti;

(b) Mbunge wa Jimbo kama Mjumbe;

(c) Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kama Mjumbe;

(d) Makatibu wa CCM wa Matawi katika Jimbo kama Wajumbe;

(e) Wajumbe wa Serikali ya Jimbo kutoka kila Tawi kama Wajumbe;

(f) Afisa wa Kilimo, Mifugo wa Jimbo kama Katibu.

Kazi za Kamati

11. Kazi za Kamati za utekelezaji wa Kilimo zitakuwa ni kuhakikisha ufanikishaji na madhumuni yaliyomo katika Sheria hii katika eneo lake na zaidi kila Kamati itakuwa na wajibu ufuatao:-

(a) Kuhakikisha kuwa ardhi yote inalimwa ipasavyo ili kuhakikisha utekelezaji wa mpango wa MTAKULA kulingana na utaratibu uliowekwa;

(b) Kuhakikisha kuwa malengo ya uzalishaji yaliyowekwa yanafikiwa;

(c) Kuwakilisha kwa Kamati iliyojuu yake ripoti zote za ufanisi au za kuwepo kwa ugumu katika utekelezaji wa kilimo katika eneo lake;

(d) Kushirikiana na Kamati nyenginezo zote pamoja na vyombo vyenginevyo vya Chama au Serikali katika uzalishaji, ukusanyaji (uvunaji), ugawaji na uuzaji wa mazao ya kilimo, na

(e) Kuchukua hatua za kuepusha wizi au uharibifu wa aina yoyote wa mazao.

Uanzishwaji wa Sekretarieti ya uratibu

12.(1) Inaanzishwa Sekretarieti itayojulikana Sekretarieti ya uratibu ambayo kazi zake itakuwa ni kuratibu shughuli za Kamati katika utekelezaji wa MTAKULA.

(2) Sekretarieti itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Katibu Mkuu - Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili kama Mwenyekiti;

(b) Mkuu wa Elimu kwa wakulima kama Katibu;

(c) Wakurugenzi wote wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili kama Wajumbe;

(d) Afisa Mdhamini wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Maliasili Pemba kama Mjumbe;.

Ushauri wa kitaalamu

13. Bila ya kuathiri masharti ya Sheria nyengine yoyote, Afisa wa Kilimo na Mifugo, Afisa wa Uvuvi na Afisa wa Misitu wanaweza kutoa ushauri wa kitaalamu kwa mtu yeyote katika shughuli za utekelezaji wa mpango wa MTAKULA.

Taratibu za Mikutano

14. Kamati au Sekretarieti itajiwekea taratibu zake za mikutano;

Isipokuwa ifahamike kwamba mikutano yoyote ile itafanyika pale tu ambapo idadi ya wajumbe itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe wote.

Usajili

15. Bila ya kuathiri Sheria nyengine yoyote kwa madhumuni ya urahisishaji wa mpango wa MTAKULA, Waziri ataanzisha na kuweka rejista ya watu wote wa Zanzibar wanaoweza kufanya kazi chini ya mpango huu kwa mujibu wa kifungu cha 2 cha Sheria hii.

(2) Regista litawekwa na kusajiliwa kwa kila mkaazi wa Zanzibar juu ya mambo yafuatayo:-

(i) Jina la Mkaazi;

(ii) Anuani;

(iii) Umri;

(iv) Idadi ya watu wanaomtegemea kama wapo;

(v) Kazi aliyoajiriwa/ anayofanya kama anayo;

(vi) Makaazi yake;

(vii) Uraia;

(viii) Makaazi ya Wazee wake.

(3) Rejista litawekwa na kusajiliwa maelekezo katika hali na namna ambayo Waziri ataeleleza.

(4) Wakuu wa Wilaya, Maafisa Tawala wa Wilaya na Maafisa wengine wanaoteuliwa na Waziri watasimamia usajili wa wakaazi katika Wilaya zao.

Utambulisho

16. Bila ya kuathiri Sheria nyengine yoyote, Waziri anaweza kuweka Kanuni za kuelezea taratibu za kutoa vitambulisho kwa watu waliosajiliwa na wanaotekeleza mpango wa mtakula.

Makosa

17. Mtu yeyote ataeshindwa kutekeleza maagizo yaliyomo katika Sheria hii, au ataewashawishi watu wengine kutotekeleza maagizo yaliyomo katika Sheria hii, au kwa nia mbaya akifanya makusudi kitendo chochote kitachosababisha uchafuzi katika kufikia malengo yaliyomo katika Sheria hii atakuwa ni mkosa na endapo Mahkama itathibitisha kosa hilo atapelekwa Chuo cha Mafunzo kwa muda usiozidi miaka miwili au atatozwa faini isiyozidi Shilingi Elfu Tano (5,000/=) au atapewa adhabu zote mbili.

Kanuni

18.(1) Waziri anaweza kuweka Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa vifungu vya Sheria hii.

11/.....

(2) Waziri anaweza kuziruhusu Serikali za Majimbo kuweka Kanuni kwa ajili ya utekelezaji bora wa Sheria hii katika maeneo yao.

Ufutwaji wa Sheria Namba 2 ya 1974.

19. Sheria ya Uongezekaji wa Mazao ya Kilimo Namba 2 ya 1974 (The Increase in Agricultural Production Decree, No.2 of 1974) inafutwa.

Imepitishwa na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar tarehe 18 Juni, 1988.

ABDUL RAHMAN ALI SALEH
KATIBU BARAZA LA WAWAKILISHI LA ZANZIBAR